

Insha

Jina: Felix Ngugi  
Shule: Shule ya msingi ya starehe

6/1/21

2

## MAJI

Maji ni kiowevu kinachopatikana kutokana na mvua katika bahari, maziwa, mito na kadhalika ambacho hutumika kwa kupikia, kunywa au kuogea. Maji ni uhai na hakuna kiumbe chochote kile kinachoweza kuishi bila maji, si binadamu, si mahayawani bali pia mimea ambayo hutusaidia sisi insi kwa njia si haba.

Maji ni muhimu kwa njia chekwa. Moja kati ya umuhimu wa maji ni kunywa.

Mahuluku na mahayawani hunywa maji ili kukata kiu. Haweza piga falaki jinsi au shi ya kiumbe chochote kile yangetokuwa bila maji. Bila shaka, maisha yangetokuwa bila mfano wowote na hakuna chochote kingeweza kuishi duniani.

Pia maji hutumika kwa kutayarisha chakula ambacho huliwa na insi ili kumweka akiwa uhai. Bila maji hatungeweza kutayarisha chakula na basi hatungekuwa uhai.

Bila kusahau, maji pia hutumika kwa kuoga na kupiga mswaki. Njia hizi mbili za matumizi ya maji hutumika kudumisha usafi wa mwili na wa mazingira. Mazingira huremba mandhari ya nchi na hivyo kuwavutia watalii. Hawa watalii wanapozuru nchi yetu, wao huja na fedha ambazo huchangia kwa kupeleka uchumi wa taifa mbele. Kwa hivyo bila maji ni bayana kuwa hatuwezi kuwa na mazingira na pasipo mazingira hapana watalii.

Maji hutumika kukuza mimea. Bila maji, mimea haiwezi kukua. Miti ni mojawapo ya mimea muhimu mno. Miti mingi pamoja hutengeneza msitu.

Misitu huchangia kuvuta mvua. Maji pia hutumika kwa kilimo. Tunapofanya kilimo ndipo tunapopata chakula. Kwa hivyo kama hakuna maji, hakuna kilimo na bila kilimo hatuwezi kupata dishi.

Isitoshe, maji hutumika kwa burudani kama kuogelea. Kuogelea huwasaidia vijana kujiepusha na mambo mabaya kama utumiaji wa mihadarati na mambo mengine mengi ya anasa. Pia kuna mashindano ya kuogelea ambayo huwapa vijana fursa ya kushiriki na kwa hivyo wao hujiepusha na mambo mengi sana yasiyo na umuhimu.

Maji hutumika katika usafirishaji kutoka ng'ambo moja hadi nyingine. Kama hakuna maji, vyombo kama vite; meli, jahazi, manowari, nyambizi na vyombo vingine vingi vya majini haviingeweza kupitia majini.

Waja wengi hukata miti kivoloya bila kupanda mingine ilhali wanafahamu fika kwamba wanapoikata wanaharibu misitu ambayo ni vyanzo vya mito. Serikali inafaa kuchukua hatua kali na kuwaadhibu insi wanaoharibu misitu oyo oyo.

Ni muhimu kulinda vyanzo vya mito kama misitu ili tupate maji ya kutosha. Tusipofanya hivyo, nchi yetu itapoteza mandhari yake na kuwa jangwa ambalo hata hakuna mja yeyote anaweza kuishi. Tunafaa kupanda miti kwa wingi ili tupate maji kwa wingi na tukuze kauli mbiu, 'kata miti mmoja lakini upande miwili au zaidi.'